

## **JIHESHIMU UHESHIMIWE**

1. Nakuita muadhamu, itikia kwa nidhamu  
Kukusema nina hamu, ukae ukifahamu  
Tafadhali jiheshimu, na watu wakupheshimu  
Tafadhali jiheshimu, na watu wakupheshimu
2. Nani atakupheshimu, kama hutajiheshimu  
Kwanza ujiheshimu, na ndipo tukupheshimu  
Hivyo ukijiheshimu, sisi tutakupheshimu  
Tafadhali jiheshimu, na watu wakupheshimu
3. Kama wewe ni mwalimu, ambaye una elimu  
Usiwe mtu dhalimu, uheshimu ualimu  
Hata kama u-mwalimu, usiringie elimu  
Tafadhali jiheshimu, na watu wakupheshimu.
4. Wanafunzi kujihimu, kwa elimu ni muhimu  
Ukijali majukumu, ya watu kuwahukumu  
Lazima ujiheshimu, na wao wakupheshimu  
Tafadhali jiheshimu, na watu wakupheshimu.
5. Pia ukiwa hakimu, usipende kujikimu  
Ukijali majukumu, ya watu kuwahukumu  
Lazima ujiheshimu, na wao wakupheshimu  
Tafadhali jiheshimu, na watu wakupheshimu
6. Unapotoa hukumu, kutimiza majukumu  
Uepuke kudhulumu, watu wasikulaumu  
Na heshima ni muhimu, kwa hivyo ujiheshimu  
Tafadhali jiheshimu, na watu wakupheshimu
7. Kwa kweli ujiheshimu, uweke mbele nidhamu  
Isitoshe ujihimu, na tena uwe na hamu  
Heshimu kitu muhimu, kwa hivyo ujiheshimu  
Tafadhali jiheshimu, na watu wakupheshimu
8. Beti nane zimetimu, sasa nazima stimu  
Na ukiwa kama timu, nadhani utahitimu  
Yote yaliyomo humo, moyoni mwako yadumu  
Tafadhali jiheshimu, na watu wakupheshimu

***Kindi Y. Abdallah***  
***September 2002***